**Hotuba ya Mwenyekiti Mtendaji Hassan Maajar Trust, Bi. Zena M Tenga Katika Hafla ya Kukabidhi Madawati, Mkoa wa Singida; Tarehe 27th Aprili 2013, Singida. Shule ya Msingi**
---------------------------------------------------------------------------------------------

***Mh.Mkuu wa Mkoa wa Singida Dr. Parseko V Kone, Ndugu Liana Hassan Katibu Tawala wa Mkoa. Mwalimu Queen Mlozi, Mkuu wa Wilaya ya Singida, Muheshimia Salum Mahami, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Singida, Mh. Celestine Yunde, Mweyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida, Bibi Iluminata Mwenda, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Wilaya ya Singida, Bibi Helen Mselle, Kaimu Mkurugenzi wa Manispa ya Singida, Mr. Neheamia Mchechu Director General NHC, ,Wenyekiti serikali za mtaa, Afisa elimu, Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Munisa, Mwenyekiti kamati ya shule, Viongozi wote wa serikali, wazazi, wanafunzi, wana habari*** **. Naomba pia kuwatambua nilioandamana nao, Bw. Shariff Maajar, Makamu Mwenyekiti wa Hassan Maajar Trust na Balozi Bertha Somi, Mwenyekiti Kamati ya Madawati au kwa jina alilopatiwa, Mama Madawati.**

**MHESHIMIWA MKUU WA MKOA**

Naomba nichukue fursa hii, kwa niaba ya uongozi wa Hassan Maajar Trust nilioandamana nao na kwa niaba ya Boadi ya Wakurugenzi wa HMT, kukushukuru sana pamoja na timu yako kwa kutupokea na kwa kupanga muda katika ratiba yako kushiriki katika zoezi hili la kukabidi madawati. Tunajua wewe ni mtu mwenye kazi nyingi lakini kwamba umechagua kuwa nasi ni dhahiri kama sisi unathamini kazi yetu. Ahsante sana Mheshimiwa.

Naomba kusema pia asante Singida kwa ukarimu wenu na kwa kutupokea vizuri.

**Hassan Maajar Trust ni nini?**

Hassan Maajar Trust ni Wakfu kwa kumbukumbu ya kijana wetu mpendwa Hassan Shariff Maajar, aliyefariki dunia Novemba 2006. Kama tunavyofahamu, Wakfu ni kitendo cha kuweka utaratibu wa kuweza kufanya shughuli za kijamii kwa manufaa ya jamii bila kutegemea malipo au faida yeyote, bila kubagua mtu kwa msingi wa dini, kabila, rangi au itikadi. Aidha Wakfu ni aina ya sadaka ambayo shughuli zake zinahitaji moyo wa kujitolea. Kwetu sisi Wakfu huu tumeuchagua kama namna ya kumkumba Hassan kwa kutoa sadaka endelevu.

Hivyo basi **HMT** imeandikishwa kama kampuni au NGO isiyo na hisa na yenye kudhaminiwa na itafanya kazi za hisani bila kugawa faida au kuwanufaisha wadhamini au wakurugenzi wake.

**Malengo ya HMT**

Lengo kuu la Hassan Maajar Trust ni kuboresha mazingira ya kusomea watoto katika shule za Tanzania. Tunahamasisha jamii kutambua wajibu wa kuchangia ili kuweka mazingira ya shule zetu kuwa mahali bora kwa watoto wetu kusomea. Katika kutimiza lengo hili, Wadhamini waliamua kwamba mahali pazuri pa kuanzia ni kushughulikia tatizo sugu la ukosefu wa madawati mashuleni. Hivyo basi waliamua kuzindua kampeni ya kwanza inayoitwa **'Dawati Kwa Kila Mtoto' (A Desk For Every Child)**

**Kwanini Singida?**

Ndahani wengi wenu mtakuwa mnajiuliza kwanini Singida?

Mwaka juzi Desemba, Hassan Maajar Trsut ilifanya hafla ya chakula cha usiku. Kwenye halfa hiyo tuliweza changisha watu fedha za mfuko wa madawati, na ni kwenye ghafla hii, tulifanya Bahati nasibu ya kuchagua mikoa 5 ambayo taasisi

yetu tutaanza nayo kazi. Singida ilikuwa kati ya hiyo mikoa 5 mengine ni Mtwara, Rukwa, Mwanza na Njombe. Leo hii Singida inapata madawati 264 kwa shule saba (7) katika wilaya Mmoja, Wilaya ya Singida. Idadi hii itawezesha wanafunzi takribani 750 ambao kwa sasa walikuwa wakikaa sakafuni, kama wakikaa watutu tu.

NATIONAL HOUSING COOPORATION

Kama nilivyosema awali Hassan Maajar Trust inahamasisha jamii kuboresha mazingira ya Elimu. Sisi hatuna fedha zetu wenye, Kati ya wadhani wetu wa kuu ni Shirika la Nyumba (NHC). Madawati tunayoyatoa leo hii yamefadhiliwa na NHC pamoja na HMT. Napenda kumshukuru Mkurugenzi Mkuu wa NHC, Bw. Kyando Mchechu pamoja na timu yake kwa ufadhili huu uliopelekea kupatikana kwa madawati 264 yatakayokalisha watoto 750.

MHESHMIWA MKUU WA MKOA

Kuwa HMT na NHC hatuwezi kutimiza azma ya kila mtoto kuwa na dawati. Hili ni jukumu la jamii Na kwa kweli sote tumeshuhudia na **HMT** inajua kwamba zipo jitihada za wengi ikiwa ni pamoja na Serikali, mashirika ya umma na watu binafsi, kukabili upungufu wa madawati, Lakini tatizo limeendelea. Na sisi HMT tunajua hatuwezi kulitatua hili tatizo peke yetu. Na ndio maana wenzetu NHC walituunga Mkono kuwezesha Singida kupata idadi nzuri ya madawati. Hivyo naomba  kutoa wito kwa wananchi wa Singida kuendelea kuchangia juhudi za kuhakikisha watoto wetu kwamwe hawatakaa tena sakafuni au kukalia vitu vya ajabu kama mawe na matofali.

**Mwisho**

Mwisho napenda kusema asante kwako Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa kukubali kushiriki hafla hii. Tunawashukuru pia viongozi wa Mkoa Ngazi mbalimbali wakiongozwa na RAS Bw. Liana Hassan kwa ushuirikiano wenu. Aidha Mkurugenzi wa NHC, Bw, Mchechu, pamoja na uongozi wa NHC Mkoa wa Singida. Mmetusaidia sana. Ahsanteni. Nawashukuru pia wadau wote mliopo mkiwepo waandishi wa habari na wananchi kwa ujumla. Si rahisi kumtaja kila

mmoja maana mwisho nitasahau wengine ikawa lawama. Nasema tu ahsanteni sana.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza**

**Mungu awabariki sana na Mungu ibariki Tanzania.**